# JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA NOVEMBA 2024







JARIDA LA RS
RUVUMA
TOLEO LA
NOVEMBA 2024



## KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA NOVEMBA 2024

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

# TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## KATIBU TAWALA RUVUMA AKAGUA MIRADI NYASA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, pichani katikati Ndugu Mary Makondo, akiwa na Kamati ya Usalama ya Mkoa, amefanya ziara ya kikazi wilayani Nyasa. Lengo la ziara ni kutembelea miradi ya maendeleo na kutoa miongozo ya kuimarisha ulinzi na usalama.

Katibu Tawala akiwa wilayani Nyasa ametembelea Hospitali ya Wilaya ya Nyasa, na kukagua jengo la wagonjwa wa nje, ambalo limejengwa kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi,pia amekagua jengo la dharura , ambalo linahusisha huduma za haraka kwa wagonjwa wanaohitaji matibabu ya Dharura.

Pia ametembelea jengo la oksijeni ambalo linahudumia wilaya za Mbinga, Ludewa, pamoja na wilaya ya Nyasa. Jengo hili limekuwa na mchango mkubwa katika kutoa huduma ya oksijeni kwa wagonjwa wanaohitaji matibabu ya papo kwa papo, yanayohitaji hewa ya Oksijeni




***Pichani kulia ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Mary Makondo akipata maelezo kuhusu miradi ya afya inayotekelezwa katika hospitali ya Wilaya ya Nyasa iliyopo Nangombo Mbambabay.***

Akiwa katika Kata ya Mpepo,Makondo ametembelea mpaka wa Tanzania na Msumbiji, eneo ambalo limekuwa na umuhimu mkubwa katika masuala ya usalama na ushirikiano wa kikanda.

Akizungumza na wananchi amewataka wananchi kuwa macho na kuhakikisha wanatambua na kutoa taarifa mapema kuhusu mgeni yeyote wasiyemfahamu, hasa wale wanaoingia au kutoka kupitia mpaka huo.

"Usalama wa mipaka yetu ni jukumu la kila mmoja wetu. Tunahitaji ushirikiano wa karibu kati ya wananchi na vyombo vya usalama ili kudumisha amani na kuzuia uhalifu katika maeneo yetu," amesisitiza Katibu Tawala huyo.

Amehitimisha Ziara yake kwa kutembelea na kukagua ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Mpepo, ambacho kinatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha usalama katika wilaya ya Nyasa.

# VIJANA WAASWA KUJIHADHARI NA MAAMBUKIZI MAPYA YA HIV



NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga, amewataka vijana hususani wasichana kuongeza juhudi katika kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Ametoa rai hiyo wakati akitoa hotuba katika kilele cha wiki ya vijana kilichofanyika katika uwanja wa Majimaji mjini Songea kuelekea maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani ambayo yatafanyika Disemba Mosi, mkoani Ruvuma.

"Ninawasihi vijana wote nchini hususani wasichana kuongeza juhudi katika kujikinga na maambukizi ya VVU, Kwa mlioko shuleni na vyuoni wekeni mkazo katika Elimu na kujiepusha na tabia zote hatarishi zinazopelekea kupata maambukizi ya VVU," alisema Mhe.Ummy.

Amewashauru vijana kushiriki katika michezo mbalimbali ili kuimarisha afya na kupata ajira kupitia michezo hiyo na kujiondoa kwenye mazingira hatarishi ya kupata VVU.

Naye Mwenyekiti wa Mtandao wa Vijana wanaoishi na VVU, Pudensiana Mbwiliza, amesema kama vijana wanaunga mkono dira ya Taifa na dunia ya kufikia kizazi kisicho na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, vifo 0 na unyanyapaa 0 ifikapo mwaka 2030.

Amebainisha kuwa takwimu za utafiti wa viashiria vya UKIMWI Tanzania (THIS) kwa mwaka 2022/23 zimeonyesha kwa kiasi kikubwa jinsi maambukizi ya VVU yanavyoendelea kuwakabili vijana hasa wenye umri wa miaka 15-24 huku kundi kubwa zaidi likiwa ni wasichana.

## CHAMA CHA MAKINI CHAPONGEZA UCHAGUZI




Katibu Mkuu wa Chama cha Makini, Ameir Hassan Ameir, amepongeza uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27 mwaka huu, akisema ulikuwa huru na wa haki.

Amesema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za Chama chao zilizopo kata ya Mjimwema mjini Songea.

“Tumesimamisha wagombea, na hakuna hata wakala mmoja aliyeleta ripoti kama kumetokea kasoro, kwa niaba ya chama Taifa, nikiwa kama Katibu Mkuu, naomba niseme kwamba uchaguzi huu wa Serikali za mitaa, vijiji pamoja na vitongoji ulikuwa huru na wa haki.” alisema Ameir.

Amekishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kushirikiana na vyama vingine vyote kuhakikisha uchaguzi unakuwa wa amani na utulivu kwani hata matokeo yaliyotangazwa ni wananchi walitumia haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi wanaowataka.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Makini Tanzania bara, Grace Ngonyani, amewapongeza wananchi wote kwa kutumia haki yao ya kikatiba kwa kuwachagua viongozi watakaowaongoza katika mitaa, vijiji na vitongoji, pia, ameushukuru uongozi wa mkoa wa Ruvuma kwa ushirikiano mzuri walioupata katika ngazi zote walizopita.

Katibu wa Chama cha Makini Mkoa wa Ruvuma, Abdalla Ngonyani, amebainisha kuwa katika mkoa mzima wa Ruvuma, chama chao kilifanikiwa kuweka wagombea katika mitaa yote 123, kati ya vijiji 551 walifanikiwa kuweka wagombea katika vijiji 308 na kuweka wagombea katika vitongoji vyote 178.

# WENGI WAJITOKEZA KUPIGA KURA UCHAGUZI SERIKALI




Baadhi ya wananchi wa Mji wa Mbinga wakiwa kwenye foleni ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika nchini kote Novemba 27 mwaka huu




Mjumbe wa Halmashauri Kuu CCM Taifa Ndugu Mohamed Aboud Mohamed akuzungumza wakati anahitimisha kampeni za uchaguzi wa Serikali za mitaa za CCM Mkoa wa Ruvuma kwenye viwanja vya Kata ya Ruvuma Manispaa ya Songea



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Mary Makondo akipiga kura ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa katika kituo cha Shule ya msingi Majimaji Manispaa Songea.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amewaongoza wananchi wa Mji wa Songea kupiga kura za kuwachagua viongozi wa mitaa kwa kupiga kura katika Mtaa wa Mshujaa Kata ya Mjini Manispaa ya Songea

## RUVUMA YAZALISHA MAZAO TANI ZAIDI YA MILIONI MBILI



Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mheshimiwa Kapenjama Ndile, amebainisha kuwa hadi kufikia mwezi Julai, 2024 Mkoa wa Ruvuma umezalisha tani 2,052,449 za mazao ya chakula.

Amesema hayo wakati akifungua kongamano la kilimo biashara lililofanyika katika ukumbi wa kanisa Katoliki Parokia ya Bombambili mjini Songea akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed.

"Nchi imezalisha tani Milioni 8, Mkoa wa Ruvuma tumezalisha tani Milioni 2 unaweza kuona sisi sio wadogo tuna mchango mkubwa katika sekta ya kilimo" alisema Kapenjama Ndile.

Katika kongamano hilo Maafisa Ugani wamepatiwa Vishikwambi kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kuongeza tija katika kilimo, ambapo amewataka Maafisa hao kuvitumia vifaa hivyo vinavyotolewa na Wizara ya Kilimo vikiwemo Vishikwambi na pikipiki kwa matumizi sahihi na yaliyokusudiwa.

Naye Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndg. Jumanne mwankhoo ameliyataja lengo la kongamano ni kujiweka sawa kuelekea msimu wa kilimo 2024/25 ndio sababu ya wadau mbalimbali wa kilimo yakiwemo Makampuni ya wauzaji wa pembejeo na mbolea kujumuika.

Ameeleza kuwa kilimo biashara ni kilimo kinachotoa faida, hivyo amewasisitiza wakulima kuweka mipango ya kilimo mapema na kuacha kulima kwa mazoea.

Kwa upande wake Afisa Kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Onesmo Ngao, ameishukuru Selous FM kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuandaa kongamano la kilimo biashara na kulitaja kama kielelezo na chachu kwa wakulima hususani kuelekea katika msimu mpya wa kilimo.

Kongamano la kilimo biashara kimefanyika mara ya pili mwaka huu ambapo mara ya kwanza lilifanyika mwaka 2023 ikiwa ni sehemu ya juhudi za wadau wa kilimo kuboresha mbinu za uzalishaji na kuongeza tija katika sekta ya kilimo.




## DED MADABA AWAFARIJI WAGONJWA HOSPITALI




Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Madaba Sajidu Idrisa Mohamed ametembelea hospitali ya Wilaya ambako huduma za kibingwa na amegawa vitafunwa kwa wagonjwa wanaosubiri huduma za kibingwa




*Baadhi ya majengo katika hospitali ya Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma ambayo imeanza kutoa huduma za matibabu kwa wananchi wa Jimbo la Madaba na maeneo Jirani*

## MBINGA YAKUSANYA MAPATO YA NDANI YA BILIONI 2.9



HALMASHAURI ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma,katika kipindi cha miezi mitatu Julai hadi Septemba 2024 imekusanya zaidi ya Sh.bilioni 2,964,142,561 sawa na asilimia 35 kati ya lengo la kukusanya Sh.bilioni 8,400,000,000 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Andrew Mbunda amesema hayo ,kwenye kikao cha robo ya kwanza cha Baraza la madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri hiyo.

Amesema ,hadi tarehe 30 Septemba Halmashauri imepokea Sh.bilioni 7,042,293,300 sawa na asilimia 26 ya makisio ya Sh.bilioni 27,227,634,000.00 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Sh.bilioni 1,769,097,000 kati ya Sh.bilioni 2,536,195,000.00kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Amesema ,ongezeko hilo ni baada ya kupokea Sh.bilioni 1,417,962,000.00 kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za mitaa unaotarajia kufanyika tarehe 27 Novemba kwa ajili ya kuwapata viongozi wa vitongoji na vijiji.

Mbunda amesema, Halmashauri imepokea jumla ya Sh.bilioni 3,291,768,549 kati ya Sh.bilioni 9,918,358,720 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za kijamii na kuharakisha maendeleo ya wananchi waliopo katika Halmashauri hiyo.

Kwa upande wake Mkuu wa wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Kisale Makori,amewapongeza watumishi na madiwani wa Halmashauri ya wilaya Mbinga kwa kazi nzuri ya kutekeleza miradi na kusimamia shughuli za maendeleo ikiwemo zoezi la uandikishaji wananchi katika Daftari la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za mitaa.

Makori aliyewakilishwa na kaimu Katibu tawala wa wilaya hiyo Karim Mzee,amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanachangia chakula kwa ajili ya watoto wao waliopo shuleni badala ya kazi ya kutoa chakula kuachwa ifanywe na Serikali.



*Baadhi ya waheshimiwa madiwani wa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wakiwa kwenye cha Baraza la madiwani*

# TANROADS KUKAMILISHA BARABARA YA AMANIMAKORO



WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Ruvuma, umewahakikishia wakazi wa wilaya za Mbinga na Nyasa wanaotumia barabara ya Amanimakoro-Ruanda yenye urefu wa kilometa 35 kuwa,ujenzi wa barabara hiyo unaendelea na itakamilika mwaka 2025.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Saleh Juma, baada ya kukagua ujenzi wa barabara hiyo inayojengwa kwa kiwango cha lami na Mkandarasi kampuni ya China Railway Sevent Group(CRSG) kwa gharama ya Sh.bilioni 60.4.

Amesema,barabara ya Amanimakoro-Ruanda ni ya kimkakati na muhimu kwa uchumi wa mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla kwani inaunganisha wilaya ya Mbinga,Nyasa na mkoa jirani wa Njombe na inatumika kusafirisha makaa ya mawe kutoka Ruvuma kupeleka mikoa mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Saleh kwa sasa kazi ya ujenzi inaendelea vizuri na kwamba matarajio ya Serikali barabara hiyo itakamilika haraka ili wananchi waweze kuitumia kwenye shughuli zao za usafiri na usafishaji.

Amesema,barabara hiyo ni sehemu ya barabara ya Kitai-Ruanda hadi Lituhi kuelekea Mbambabay wilayani Nyasa kupitia Bandari ya Ndumbi,ambapo Serikali iko katika maandalizi ya kujenga kipande kingine kutoka Ruanda hadi Lituhi kwa kiwango cha lami.

“kimsingi kazi inayofanywa na mkandarasi ni kuandaa lea ya kwanza na pili kabla ya kuweka lami,mpango wetu kwa mwaka huu 2024 tuwe na lami yenye urefu wa angalau kilometa tano,nachukua nafasi hii kuwaeleza wananchi wa mkoa wa Ruvuma kwamba, Mkandarasi yuko saiti na kazi inaendelea"alisema Saleh.

Amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha zilizowezesha ujenzi wa barabara hiyo kuendelea na kuhaidi kumsimamia mkandarasi ili aweze kukamilisha ujenzi kazi kwa wakati kwani kuwa barabara hiyo inategemewa sana kuharakisha maendeleo na uchumi wa mkoa wa Ruvuma.

Msimamizi wa kitengo cha ndani kutoka TANROADS Mkoa wa Ruvuma Andrew Sanga amesema,mradi huo unahusisha ujenzi wa madaraja makubwa manne kati ya madaraja hayo, matatu ujenzi wake unaendelea ambapo moja limekamilika. Kwa mujibu wa Sanga,ujenzi wa daraja la pili uko hatua za mwisho na mkanadarasi anamalizia kufunga nondo kabla ya kumwaga zege juu,na mategemeo ya wakala kwamba ujenzi wa madaraja yote yatakamilika kwa wakati.

Meneja mradi wa Kampuni yaCRSG amesema,kazi ya kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa tano inaendelea vizuri na itakamilika ifikao mwezi Fabruari mwakani.

Baadhi ya wananchi,wameipongeza Serikali ya awamu ya sita kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo ambayo inakwenda kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi na kurahisisha usafiri kati ya vijiji vya kata ya Amanimakoro na maeneo mengine ya wilaya ya Mbinga na mkoa wa Ruvuma.

## WADAU WA KILIMO WATAKIWA KUTOA ELIMU SAHIHI YA PEMBEJEO ZA KILIMO



Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Ndugu. Jumanne Mwankhoo amewataka wadau wa kilimo kutoa Elimu sahihi ya matumizi ya pembejeo za kilimo kwa wakulima ili waweze kupata matokeo mazuri.

Amesema hayo wakati akifungua kikao cha wadau wa kilimo kuelekea msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2024/25 kilichowajumuisha maafisa kilimo na wauzaji wa pembejeo za kilimo kilichofanyika katika ukumbi wa Heritage Cottage mjini Songea.

"Niwasihi wadau wote wa kilimo tuendelee kushirikiana ili kuhakikisha elimu sahihi inafika kwa wakulima, niwaombe wauzaji wa pembejeo tuwashauri wakulima ipasavyo, tusiwashauri tu kwa maana ya tunataka tuuze,"alisema Ndg. Mwankoo.

Nae Afisa kilimo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Onesmo Ngao, amesema tayari wametoa vibali kwa Makampuni na wadau wa kilimo kutoa Elimu kwa wakulima katika Halmashauri.

Ameongeza kuwa suala la Elimu ni mtambuka hivyo wadau wote wanatakiwa kwenda kwenye maeneo ya kazi na kuwafikia wakulima ili kutoa Elimu.

Kwa upande wake Mkaguzi wa Mbegu kutoka Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Kapaya Said, ameeleza namna ambavyo Serikali imekuwa

ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha wafanyabiashara wanauza mbegu boraa na sahihi.

Ameongeza kuwa mbegu zote za mahindi za msimu wa kilimo wa 2024/25 zinatakiwa ziwekwe katika mfumo wa kidijitali na kuuzwa kwa mfumo wa ruzuku ambapo tayari Makampuni ya uuzaji wa pembejeo yanaendelea kuweka mbegu katika mfumo huo.

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa inayoongoza kwa shughuli za kilimo hususani uzalishaji wa zao la mahindi.



## SOKO LA KILOSA MBAMBABAY LATEKETEA KWA MOTO



Soko la Mbamba bay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma limeteketea Kwa moto usiku wa kuamkia Tarehe 16/11/2024 na kuuunguza vibanda 25 vya soko hilo na mali ambazo zilikuwepo katika vibanda hivyo.

Mashuhuda wamesema kwamba majira ya saa tisa usiku waliona moto ukiwa unawaka katika soko hilo ambapo kila duka lilikuwa na mali.

# RUVUMA KUPANDA MITI YA KIBIASHARA HEKARI 100,000



Mkoa umekuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii juu ya upandaji miti na utunzaji mazingira.

Uhamasishaji huu huenda sanjari  na utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji miti ambao hufanyika kila mwaka kwenye Halmashauri zote.

Mkoa wa Ruvuma una lengo la kupanda miti kibiashara ekari 100,000 kwa muda wa miaka kumi (10) toka 2015 – 2025.

Mradi huu utatekelezwa katika maeneo ya Serikali, vyuo na shule,Kwa msimu wa mwaka 2023/24 Mkoa wa Ruvuma umepanda jumla ya miche ya miti **4,099,014** ambapo imepandwa katika Halmashauri zote, miti hii ni kwa ajili ya mbao, vyanzo vya maji na matunda.



# BILIONI 16.2 KUJENGA BARABARA YA LAMI UTIRI MBINGA



Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, MKOA Ruvuma Mheshimiwa Kisare Makori, amebainisha kuwa kiasi cha shilingi Bilioni 16.2 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa Kilomita 14.41 kutoka kata ya Utiri hadi Mahande iliyopo katika Wilaya ya Mbinga, Mkoani Ruvuma.

Amebainisha hayo wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed katika hafla ya makabidhiano ya mradi wa ujenzi wa barabara hiyo kwa Mkandarasi Ovans Construction Limited iliyofanyika katika kata ya Utiri Wilayani Mbinga.

"Hizi si fedha kidogo, na sisemi kwamba kazi ni ndogo, tufanye kazi usiku na mchana, mjitahidi kwa kadri mtakavyoweza wewe na timu yako ili kazi iweze kukamilika kwa wakati," alisema Mhe. Kisare.

Amemsisitiza Mkandarasi wa mradi huo kuifanya kazi hiyo kwa ubora zaidi ili mradi uweze kufanana na matarajio ya wananchi wa kata ya Utiri.

Naye Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Jumanne Mwankhoo, ametoa rai kwa wote watakaopata nafasi za kufanya kazi katika mradi huo kuwa waadilifu na kujiepusha na hujuma kwenye mradi.

Amemsisitiza Mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha anakamilisha mradi huo ndani ya miezi 18 kama ilivyo kwenye mkataba na kwa ubora mkubwa ili thamani ya fedha iweze kuonekana na manufaa makubwa ya mradi huo yaweze kupatikana kwa wananchi.

Kwa upande wake Mkandarasi wa mradi huo Mhandisi Valence Urio ameahidi kwenda kutekeleza mradi huo kwa wakati na kwa kufuata mkataba wa miezi 18.

## SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA RUVUMA YAIMARIKA



Mkoa wa Ruvuma umeendelea kupiga hatua katika sekta ya viwanda na biashara ambapo Mkoa una viwanda vikubwa sita vinavyoshughulika na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Viwanda vitatu vya kukoboa kahawa vipo Wilaya ya Mbinga, kiwanda cha kubangua korosho kipo Wilaya ya Tunduru, kiwanda cha kufua umeme kipo Wilaya ya Songea, na kiwanda cha kusindika unga wa sembe kipo Wilaya ya Songea.

Mbali na viwanda hivyo vikubwa, Mkoa wa Ruvuma una viwanda vya kati 25 vinavyoshughulika na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo kama unga wa sembe, mchele, mikate, na maziwa.

Pia, Mkoa una viwanda vidogo 190 na viwanda vidogo sana 3,264 vinavyoshughulika na shughuli mbalimbali kama kukoboa na kusaga nafaka, kukamua mafuta ya alizeti, usindikaji wa mihogo, cherehani, usindikaji wa nyama, sembe, juice, useremala, na bidhaa nyingine za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, na maliasili.

Bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo huuzwa ndani ya Mkoa na mikoa jirani kama Mbeya, Lindi, Mtwara, Njombe, Dar es Salaam, na nchi jirani za Malawi na Msumbiji.

Katika sekta ya biashara, Mkoa umeendelea na zoezi la kurasimisha biashara na kutoa leseni kwa kuzingatia sheria na kanuni za utoaji wa leseni za biashara kama ilivyoagizwa na Serikali.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024, jumla ya leseni 8,370 zilitolewa na jumla ya milioni 783,926,622 zilikusanywa kama mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa leseni za biashara katika Mkoa wa Ruvuma.

Hatua hizi zinaonesha jinsi Mkoa wa Ruvuma unavyoendelea kuimarisha katika sekta ya viwanda na biashara

## BWAWA LA ASILI LILILOBONYEA LINAVYOVUTIA WENGI NAMTUMBO



Bwawa la asili ambalo limetokana na mbonyeo wa ardhi lililopo ndani ya hifadhi ya jamii Mbarang'andu wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma ni moja ya vivutio vya utalii vinavyovutia wengi.Bwawa hilo linaloitwa Kaunde limesheheni wanyama aina ya viboko na viumbe wengine na kwamba bwawa hilo halina chanzo lipo jirani  na geti la  Hifadhi ya Taifa ya Nyerere Likuyu Namtumbo

## KAMBI YA UCHUNGUZI MAGONJWA YA MACHO YAFANYIKA RUVUMA KWA SIKU KUMI



Daktari Bingwa wa Macho kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea (HOMSO) Dr. Charles Hinju, amesema wameungana na madaktari bingwa kutoka ndani na nje ya nchi kutoa matibabu ya macho kwa wakazi wa Ruvuma.

Amesema huduma hizo zinazotolewa kwa gharama nafuu kupitia shirika la EyeCorps, kwa kushirikiana na madaktari kutoka CCBRT, Hospitali ya Kanda ya Mbeya, na Muhimbili zimeanza Novemba 11 na zitamalizika Novemba 20 katika hospitali ya Mkoa.

"Tunatoa huduma kwa gharama nafuu zaidi, watu walikuwa wanakuja kwetu na wanakosa huduma kwa kukosa kuchangia gharama, lakini hawa ndugu zetu na kwa kushirikiana na Serikali imeweza kutumia hii nafasi kupunguza gharama ndio maana watu wengi wamejitokeza kupata huduma," alisema Dr. Hinju.

Ameongeza kuwa katika kipindi cha wiki moja kabla ya kuanza rasmi matibabu hayo madaktari walitembelea Vijiji vya Wilaya ya Namtumbo, Songea Vijijini, na Manispaa ya Songea, kuwachunguza wagonjwa na kufanikiwa kuwapata wagonjwa zaidi ya 1,000.

Amebainisha kuwa wanatarajia kufanya upasuaji wa mtoto wa jicho kwa watu 250, na huduma zingine kama kutoa miwani kwa wenye shida ya kuona, kusoma

maandishi, na mwanga zinatolewa, hivyo wananchi waendelee kujitokeza ili waweze kufaidika na huduma hiyo.

Mmoja kati ya wagonjwa waliopatiwa huduma ya macho Florencia John kutoka Wilaya ya Tunduru amesema amefurahishwa na huduma aliyopatiwa kwa sababu alikuwa na tatizo kwenye macho yote mawili na ameshahudumiwa jicho moja na ameanza kuona, amewaomba watoa huduma kuendelea kutoa huduma hizo kwa kuwa sio kila mtu anaweza kulipia.

Naye Selemani Sindo kutoka Wilaya ya Namtumbo ameeleza kuwa jicho lake moja lililkuwa halina uwezo wa kuona lakini baada ya upasuaji sasa anaona vizuri kwa kutumia macho yote.

Huduma hii inayotolewa na kambi ya madaktari wa uchunguzi wa magonjwa ya macho huwa inatolewa kila mwaka  ambapo mwaka 2023 wagonjwa 185 mkoani Ruvuma walipatiwa matibabu ya upasuaji wa mtoto wa jicho, na mwaka huu wanatarajia kufanya upasuaji huo kwa watu 250.



## HOSPITALI YA PERAMIHO YAZINDUA HUDUMA YA CT SCAN




Hospitali ya Rufaa ya Misheni ya Mtakatifu Joseph Peramiho iliyopo Wilayani Songea, Mkoani Ruvuma imezindua Mashine ya kutolea huduma ya mionzi (CT-Scan) kwa ajili ya kuboresha huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo Dr. Adeodatus Haule wakati akitoa taarifa ya hospitali hiyo amesema hospitali hiyo iliibua mradi wa kununua na kufunga mashine ya CT-Scan ili kuboresha huduma za upimaji wa magonjwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

"Hospitali ilipokea fedha kutoka kwa wafadhili Wamisionari Wabenedictine wa Mtakatifu Ottilian Ujerumani kiasi cha Milioni 214,288,583 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la CT-Scan, baada ya jengo kukamilika wafadhili hao walinunua mashine ya CT-Scan iliyogharimu fedha za kitanzania Shilingi Bilioni 1,550,745,000,"alisema Dr. Haule.

Amebainisha kuwa mradi huo umekamilika na huduma zimeanza kutolewa tangu Septemba 2024, baada ya kukaguliwa na wataalam kutoka Tume ya Mionzi (TAEC), na wagonjwa takribani 70 wamehudumiwa na mashine hiyo.

Hospitali ya Peramiho iliteuliwa kuwa hospitali teule ya Wilaya ya Songea mnamo Juni 25, 2010 na mwaka 2011 Wizara ya Afya ilipandisha hadhi ya huduma ya hospitali hiyo kuwa kati ya hospitali 10 za mashirika ya dini yanayohudumu katika ngazi ya hospitali ya rufaa ngazi ya Mkoa bila kuondoa makubaliano ya awali ya kuhudumia kama hospitali teule ya Wilaya ya Songea.

Ametoa tahadhari hiyo wakati anazungumza kwenye kikao cha Baraza la madiwani cha Halmashauri hiyo kilichofanyika Kilosa Mbambabay.

## TAKUKURU RUVUMA YAOKOA MILIONI 16




Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi Milioni 16,736,800 kuanzia Julai hadi Septemba 2024.

Hayo yamebainishwa na Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Janeth Haule, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya TAKUKURU Mkoa, mjini Songea.

Janeth amesema kuwa fedha hizo zimeokolewa kwa kudhibiti vitendo vya rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mbalimbali mahakamani na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Ameongeza kuwa wamefanikiwa pia kuokoa kiasi cha shilingi Milioni 2,750,000 kutoka katika ujenzi wa jengo la dharura Wilayani Tunduru, ambapo kulitokea ubadhirifu na kusababisha upotevu wa fedha hizo.

Amesema kwa kipindi cha miezi mitatu, TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imefuatilia miradi 18 ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 6,512,542,640 ikijumuisha ujenzi wa madarasa, vyoo, jengo la mama na mtoto, miundombinu ya maji, na barabara.

Amebainisha kuwa miradi miwili kati ya hiyo yenye thamani ya shilingi Milioni 962,556,000 ilikutwa na mapungufu na hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuondoa mapungufu hayo.

## RC RUVUMA ATOA POLE KWA MAJANGA YA NYASA NA DSM



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ametoa pole kwa wahanga kufuatia majanga mawili yaliyotokea nchini likiwemo la kuanguka kwa ghorofa Kariakoo jijini Dar es salaam na kusababisha vifo na uharibifu wa mali na kuungua Soko la Mbamba bay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma ambalo limeteketea Kwa moto na kuuunguza vibanda 25 vya soko hilo na mali ambazo zilikuwepo katika vibanda.



*Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga akizungumza na wananchi wa Kata ya Luchili wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma wakati anazindua rasmi kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa wilayani humo*

## WAANDISHI WA HABARI WAASWA KUZINGATIA MAADILI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewasisitiza waandishi wa habari kuendelea kuyazingatia maadili ya uahandishi wa habari na kuwaelimisha wengine ambao wanakiuka maadili hayo.

Ameyasema hayo wakati akifungua Semina ya kijamii kuhusu kukuza uhuru wa kujieleza iliyofanyika katika ukumbi wa Hospitali ya Mkoa, Songea (HOMSO) mjini Songea, ambayo iliandaliwa na Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) kwa kushirikiana na Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoani Ruvuma (RPC).

"Wale ambao mnawaona wanaenda kinyume na sheria zenu msiwaone ni maadui, endeleeni kuwakumbusha, endeleeni kuwarudisha kwenye mstari ili muendelee kuijenga tasnia ya habari katika viwango vya juu vya thamani, wachache wasiwaharibie," alisema Kanali Ahmed.

Amewakumbusha waandishi wa habari kuendelea kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27 mwaka huu ili kuwachagua viongozi ambao watashirikiana na Serikali kuleta maendeleo kwenye Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Kupitia Semina hiyo iliyowakutanisha wadau kutoka taasisi za kijamii, vyama vya siasa, viongozi kutoka Serikalini na dini pamoja na watu binafsi wenye ushawishi

## KITUO CHA AFYA MCHOTEKA TUNDURU KUPEWA AMBULANCE




Waziri wa Afya, Mheshimiwa Jenista Mhagama, amebainisha kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya na TAMISEMI wamenunua magari ya wagonjwa kwa ajili ya maeneo ambayo hayakuwa na magari ya wagonjwa kikiwemo kituo cha afya cha Mchoteka.

Amebainisha hayo wakati akizindua kampeni kuelekea uchaguzi wa Serikali za mitaa katika kata ya Mchoteka wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Mhagama ameeleza kuwa wiki mbili zilizopita alikabidhiwa gari la wagonjwa kwa ajili ya kata ya Mchoteka huku akisisitiza si kwa ajili ya Mchoteka pekee bali na maeneo mengine yenye uhitaji wa magari hayo.

“Wiki mbili zilizopita nilikuwa tayari nimeshakabidhiwa gari la wagonjwa la kata ya Mchoteka, sio gari la hapa Mchoteka tu kama kawaida ya Mhe. Rais ni hapa Mchoteka na maeneo mengine yenye shida,” alisema Mhe. Jenista.

Kupitia uzinduzi wa kampeni hizo, Mbunge wa Tunduru Kusini, Mheshimiwa Idd Mpakate, ameeleza kuwa kituo cha afya cha Mchoteka ni cha muda mrefu na kinatoa huduma mbalimbali za afya ikiwemo huduma za upasuaji.

Hata hivyo, amesema kuwa kero kubwa iliyopo katika hospitali hiyo ya kata ni kukosekana kwa gari la kubebea wagonjwa.

Serikali ya Tanzania imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili kuboresha huduma za afya nchini zikiwemo ujenzi wa vituo vya afya, utoaji wa vifaa tiba na ununuzi wa magari ya wagonjwa yakisambazwa katika vituo vya afya na hospitali mbalimbali nchini.

## WAZIRI NDUMBARO ALIVYOMNADI MBUNGE WA NYASA



Waziri wa Utamaduni,Sanaa na Michezo na Mbunge wa Songea mjini Dkt.Damas Ndumbaro akimpongeza Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya kwenye kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa katika Kata ya Tingi wilayani Nyasa ambapo uchaguzi huo ulifanyika nchini kote Novemba 27 mwaka huu.



**UZINDUZI WA KAMPENI ZA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA NGAZI YA MKOA WA RUVUMA**



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Salim Abri ASAS akiwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma Komred Oddo Mwisho wakielekea kwenye ufunguzi

wa Kampeni za CCM ngazi ya Mkoa wa Ruvuma zilizozinduliwa katika Kata ya Tingi wilayani Nyasa



## UFUNGUZI RASMI MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahamed Abbas Ahamed, amesema kuwa Mkoa wa Ruvuma hali ya maambukizi imepungua kutoka asilimia 5.6 mwaka 2016/2017hadi kufikia asilimia 4.9 mwaka 2023 sawa na asilimia 0.7ya kiwango kilichopunguwa ambapo halmashauri ya manispaa ya Songea inaongoza ikifuatiwa na halmashauri ya Tunduru.

Mkuu huyo wa Mkoa ameyasema hayo leo wakati akizindua Maadhimisho ya siku ya Ukimwi Duniani katika viwanja vya Michezo vya majimaji, ambayo Kitaifa yanafanyika Mkoani Ruvuma katika Manispaa ya Songea mgeni rasmi atakuwa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Philipo Mpango.

Kuhusu hali ya UKIMWI mkoani Ruvuma takwimu zinaeleza kuwa wanaoishi na maambukizi ya virus vya ukimwi (VVU) wapo 68,237 ambao wanaume ni 24,959 sawa na asilimia 37 ,Wanawake 43,000 sawa na asilimia 63 ,watoto chini ya umri wa miaka 15 wapo 2,382 sawa na asilimia 3.5 na watu wazima kuanzia umri wa miaka 15 wapo 65,855 sawa na asilimia 96.5.

" Ndugu viongozi pamoja na wananchi halmashauri zetu zinazoongoza ni maspaa ya Songea ikifuatiwa na Tunduru lakini vile vile na halmashauri ya Mbinga hivyo napenda kuchukuwa fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote kuzingatia tiba na matunzo lakini vile vile kuendelea kutumia dawa za kufubaza kwani hiyo njia pekee ya kuendelea kupambana na matatizo haya" alisema Kanali Ahamed Abbas Ahamed.

Alisema kuwa siku hii  ya ufunguzi ni muhimu kwa kuelimisha umma kuhusu janga la UKIMWI, kuhamasisha kupunguza maambukizi mapya, na kuongeza juhudi za matibabu na huduma kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU).

Katika uzinduzi huo, Kanali Ahamed alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa jamii, serikali, na wadau mbalimbali katika kupambana na ugonjwa huu. Hii ni sehemu ya jitihada za kitaifa kuendeleza elimu na ufahamu kuhusu UKIMWI, na kudumisha haki za watu wanaoishi na virusi hivyo.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Wizara ya Afya Dkt. Catherine Joachim Mkuu wa Program ameupongeza  uongozi wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na wananchi wake kwa kupiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi kwa ushamiri wa VVU umeshuka kutoka asilimia 5.6 mwaka 2016/17 mpaka asilimia 4.9 mwaka 2022 .

Alisema kuwa takwimu hizo zinaonesha Mkoa wa Ruvuma unaongoza katika upimaji wa VVU hata hivyo Mkoa umeendelea kufanya vizuri katika VVU vya 95/95/95 ambapo ushamiri wa utafiti wa mwaka 2023 tumeonesha asilimia 82 ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanatambua hali zao za maambukizi na asilimia 97 ya walioambukizwa wanatumia dawa za kufubaza virusi vya ukimwi na asilimia 99 ya wanaotumia dawa za kufubaza tayari wameshafubaza virusi jambo ambalo linaoneaha Mkoa huo umepiga hatua kubwa sana ikili ganishwa na mwaka 2016/17.

" Japokuwa Mkoa upo nyuma ukilinganisha na wastani wa Kitaifa wa 95/95/95 ambapo 95 ya kwanza Kitaifa tupo asilimia 83, 95 ya pili tupo asilimia 98 na 95 ya Tau tupo asilimia 94" alisema Dkt. Catherine Joachm.

Alieleza zaidi kuwa kutokana na Mkoa wa Ruvuma umeendelea kukuwa kiuchumi kupitia shughuli za kilimo ,migodi ya makaa ya mawe na madini mengine.



Waziri Mkuu Mheshimiwa kassim Majaliwa alipowasili mjini Songea mkoani Ruvuma kwa lengo la kushiriki kilele cha maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani Desemba Mosi 2024.

Mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo alikuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Philip Mpango

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**
**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**

**SIMU Nambari. 025-2602256/2602238**

**FAX Na. 2602144**

**E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz**

**TOVUTI: www.ruvuma.go.tz**

**INSTAGRAM: rs ruvuma**

**FACEBOOK: rs ruvuma**

**YOUTUBE: rs ruvuma**